**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO.**
**SHULE YA SEKONDARI KASISI**

**S.L. P 259, Urambo,**
**Mkuu wa shule. Simu Na:0626481008/0785002701**
**Makamu mkuu wa shule Utawala +255742639880**
**Makamu mkuu wa shule Taaluma + 255622667958**

Tarehe………………………..

***KUMB NA KSS/ADM/2026/01***
Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi
.........................................................................................
S.L.P.....................................................................................

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KASISI - HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO MKOA WA TABORA MWAKA……………………………**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka……………..na atasoma tahasusi ya ....................... Shule ipo katika Mkoa wa Tabora, Wilaya ya Urambo, Tarafa ya Urambo katika kata ya Kasisi.
Shule ipo umbali wa km 13 kutoka Halmashauri ya wilaya ya Urambo. Ukiwa unatoka Tabora kuja Urambo utashuka Itundu kabla ya kufika Urambo mjini kisha utachukua usafiri wa pikipiki kwa kiasi cha Tsh 3000/= hadi shuleni na ukiwa unatoka Kigoma kuja Urambo itakulazimu upite Urambo mjini kama unaelekea Tabora na kisha utashuka Itundu na kuchukua pikipiki kwa kiasi cha Tsh 3000/= hadi shuleni. Ukishuka Itundu mpaka shule ni km 4.

Muhula wa masomo unaanza tarehe……………..hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe……………….Tafadhali mwanafunzi afike siku hiyo na mzazi au mlezi bila kukosa kwa ajili ya kupokea maelekezo ya pamoja.
Kumbuka kuripoti katika ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule mara unapoingia maeneo ya shule hivyo utapokelewa na kuingizwa kwenye rejesta ya shule utakapokuwa UMETIMIZA mambo yaliyomo kwenye fomu hii na kukabidhi.

MAELEKEZO MUHIMU YALIYOPO KWENYE FOMU NI PAMOJA NA;

1. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE
3. FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE
4. FOMU YA VIPIMO VYA AFYA HOSPITALI
5. UTHIBITISHO WA NDUGU WA MWANAFUNZI
6. ORODHA YA VITABU VINAVYO TUMIKA KWA NGAZI YA ELIMU YA KIDATO CHA TANO NA SITA.

**2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -**

**2.1 SARE YA SHULE**

1. Suruali mbili rangi ya **Dark blue** zenye **malinda mawili** mbele, upana wa kuanzia cm 15
2. Shati mbili nyeupe (tetroni) za mikono mirefu zisizo bana mwili na ziwe na urefu wa kutosha kuchomekea ndani ya suruali ( **zingatia sana hili)**
3. **Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili** vya kufunga kamba
4. Soksi **nyeusi ndefu** (stocking) jozi mbili au zaidi
5. Sweta rangi ya **bluu** yenye shingo ya ( V)
6. Mkanda **mweusi** wa ngozi wa kuvalia suruali.
7. Nguo za **michezo** ( Bukta mbili)
8. T-Shirt mbili za bluu zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni.
9. Track suit ya rangi ya Dark bluu
10. Nguo za nyumbani **haziruhusiwi kabisa**

**2.2 MAVAZI YANAYORUHUSIWA UKIWA SHULENI BAADA YA MASOMO**

1. Suruali nyeusi yenye malinda na **upana** chini kuanzia **cm 15**
2. Kama una matatizo ya kifua/diptherial (Onyesha cheti cha daktari) na unaruhusiwa kuwa na sweta la blue isiyo na maandishi wala alama

**2.3 MICHANGO YA SHULE**

Michango muhimu inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

i. Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=
ii. Tahadhari 5000/=
iii. Nembo 5000/=
iv. Kitambulisho cha shule 5000/=

**JUMLA 80,000/=**

**NB:** fedha zote zilipwe kwenye akaunti namba **51310032357**, katika benki ya Nmb, jina la akaunti Kasisi secondary school capitation, (Tafadhali kumbuka kuandika jina la mwanafunzi kwenye pay- *in slip*)

### 2.4 MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI: -

1. Vitabu vya masomo ya tahasusi aliyochaguliwa kujiunga
2. Dissecting kit na gloves boksi moja kwa wanafunzi wanaosoma bailojia,
3. Scientific calculator kwa wanafunzi wote.
4. Godoro la sponji **6'' x 2.5''**
5. Madaftari nane quire 3 au 4
6. Mto mmoja na foronya mbili
7. Shuka mbili rangi ya ***bluu***
8. Blanketi moja ***nzito ya rangi ya blue*** isiyo na maua
9. chandarua moja (1) nyeupe ya pembe nne.
10. Kandambili za kuogea ( siyo sandles au yeboyebo)
11. Tranka
12. Rimu moja ya A4 kwa term
13. Vyombo vya chakula ( sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
14. Kwanja **01** au jembe **01** lenye mpini kwa PCM na blashi moja ya kusugulia chooni au bafuni zenye mkono mrefu( hardbloom)**,** na fagio laini mbili za ndani **na** ndoo kwa PCB.

### 3.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku **90** bila taarifa/utoro
Kugoma na kuhamasisha mgomo
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla.
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
v. Kufuga nywele ndefu. Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.
vi. Kufuga ndevu
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
viii. Uvutaji wa sigara
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yeyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au viambatwa vya simu kama laini, betri, chaji ya simu katika mazingira yashule
xv. Kudharau Bendera ya Taifa
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi
xviii. Kuruka wigo wa shule au kukamatwa nje ya mipaka ya shule bila kibali cha uongozi wa shule.

**Aidha**, makosa mengine ambayo hayakutajwa hapo juu, mfano: kukwepa kufanya majaribio, mahudhurio hafifu darasani, kutotii kengele, kutokamilisha kazi za darasani, kutofanya usafi eneo alilopangiwa, kuzungumza Kiswahili ukiwa eneo la shuleni n.k yatatolewa adhabu ndani ya shule.

***Mwanafunzi hataruhusiwa kutoka nje ya shule kutafuta huduma za kifedha au manunuzi yoyote isipokuwa kwa kusaidiwa na walimu wake walezi wake yaani Patron.***

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YETU.**

..................................
**NGA MABULA**
**MKUU WA SHULE**

THE HEADMASTER
KASISI SECONDARY SCHOOL
URAMBO.

## 4.0 FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

(Ijazwe na kukabidhiwa kwa msajili wa wanafunzi siku ya kuripoti shuleni kwa mara ya kwanza) 1. Jina kamili la mwanafunzi, kama lilivyo katika SELFORM (kwa herufi kubwa zote).

…………………………………………………………………………………………

2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………………………………………......
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya) …………………………………………………...
4. Uraia………………………………………………………………………………
5. Shule anayotoka ……………………………………………………..................
6. Dini ……………………………………………………………………………….
7. Dhehebu ……………………………………………………………..................
8. Nyumbani ni: Mkoa ……………………………… Wilaya…………………...
9. Jina kamili la mzazi/mlezi ……..……………………………………………...
10. Uhusiano na mlezi kama hana mzazi ………….………………………..................
11. Anuani ya mzazi/mlezi ………………………………………………………
12. Namba ya simu ya mzazi/mlezi ……………………………………………….

(Mabadiliko yawasilishwe Ofisini mara moja)

**Ahadi ya mwanafunzi.**

(a) Mimi……………………………………………………Nakubali nafasi ya shule hii niliyopewa. Naahidi kutii KIKAMILIFU sheria na kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa shule ya sekondari Kasisi, naahidi kwamba sitashiriki katika migomo, fujo na makosa mengine ya jinai, na kwamba

UTORO KWANGU UTAKUWA NI MWIKO.

(b) Ninaahidi kwamba kamwe sitachelewa kurudi shule mara likizo inapokwisha na kwamba nikichelewa nitakubali adhabu zote zitakazotolewa ikiwemo kurudishwa nyumbani n.k.

(c) Nitasoma kwa bidii ili kufikia wastani wa shule ambao mwisho ni Division III na kwamba nisipofanya vizuri katika mitihani ya ndani nitabaki shule wakati wa likizo kwa ajili ya masomo ya ziada kwa gharama za mzazi/mlezi.

(d) Kamwe sitalala Bwenini wakati wa vipindi kwani kosa hilo linaweza kunifukuzisha shule.

Saini ya Mwanafunzi …………………Tarehe……………………………………

10. <u>Ahadi ya Mzazi/Mlezi:</u>

Nakubali mwanangu ajiunge na Shule ya Sekondari Kasisi katika kidato cha ……………mwaka …… na ninaahidi kwamba NITAKUWA TAYARI KUSHIRIKIANA NA WALIMU KATIKA MALEZI YA MTOTO WANGU KINIDHAMU

Jina la Mzazi/Mlezi……………………………………………

5.0 **FOMU YA VIPIMO VYA AFYA HOSPITALI**

(To be completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster Kasisi Secondary School)
To be completed by a medical Officer in respect of all Form V entrants

Student's full name…………………………………………………………………………………….

Age/Years……………………………………Sex……………………………………….

Blood found (red and White) ……………………………………………………………

Stool examination: ……………………………………………………………………

Hearing: …………………………………………………………………………….

Urinalysis: ………………………………………………………….…………

Venereal Diseases test: ………………………………………….……………….

T.B. test: ……………………………………………………………..……………

Eye Test: ……………………………………………………………………………

Ears: …………………………………………………………………..……….

Chest: ……………………………………………………………….………

Leprosy …………………………………………………………………………………

Epilepsy …………………………………………………………………………….
Limbs: ……………………………………………………………………………………
Spleen: ………………………………………………………………….…………
Abdomen: ………………………………………………………………………….
ADDITIONAL INFORMATION (If any) e.g., Physical defects, impairment(s) e.g., arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.
……………………………………………………………………………………………..

I certify that the above is fit to pursue further education as stated above.

Signature: …………………………….

Designation: ………………………Station: …… ……………Date: ….…………………....

Official Stamp: ………………………

**TANBIHI**

a) Hakikisha mtoto anakuja na kadi ya bima ya afya, au Tsh 50,400/= kwaajili ya bima ya afya, kwasababu gharama za matibabu ni kubwa sana na ni gharama ya mzazi.

b) Kwa siku za hivi karibuni, kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu, na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.

TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA
UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KUPITIA NAMBA ZILIZOPO KATIKA FOMU HII.

**6.0 UTHIBITISHO WA NDUGU WA MWANAFUNZI**

| NA. | PICHA | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |

**SHULE YA SEKONDARI KASISI**
**ORODHA YA VITABU VINAVYO TUMIKA KWA NGAZI YA ELIMU YA KIDATO CHA TANO NA SITA.**

1. **BIOLOGY**
   (a) Understanding to biology Advanced biology
   (b) Tanzania Institute of Education Biology form V and VI
   (c) Chand Biology
2. **CHEMISTRY**
   (a) Chemistry for Secondary Schools form V and VI (TIE)
   (b) Understanding Chemistry by Ted-lister
   (c) Ramsden EN (2000) Advanced level Chemistry 4$^{th}$ edition United Kingdom
   (d) Inorganic Chemistry part A Mzumbe book project
   (e) Understanding Chemistry for Advanced level (3$^{rd}$ edition 2000) Nelson Thornes (f) East Africa chemistry for o-level.
3. **PHYSICS**
   (a) Principles of Physics Class XI and XII by S. Chands
   (b) Advanced Physics by Michael Nelkon
   (c) Fundamental of Physics by Resnick
   (d) University Physics
   (e) Understanding Physics
   (f) Advanced Physics (Roger Muncaster)
   (g) Physics for ordinary level
   (h) Understanding physics form 1-iv.

4. **ADVANCED MATHEMATICS**
   (a) S. Chand's for Class xi and xii
   (b) Pure Mathematics 1 and 2
   (c) Advanced Mathematics Tranter
   (d) Understanding Mathematics